Ushirikishaji wa Umma wa Sikiliza na Ujifunze:

Kipindi Kifupi

Maagizo

Katika kipindi hiki kifupi, tutachunguza umuhimu wa wanafunzi wetu kupata mafanikio ya kielimu na jinsi tunavyoweza kupanua fursa za kuwasaidia kufika huko.

Kila chumba kitakuwa na mwendeshaji na katibu wa kunakili mambo muhimu na mada kuu za majadiliano yenu - mikutano hii hairekodiwi, lakini uandikaji wa kumbukumbu ni muhimu ili kuwezesha Shirika kujumuisha mada za jumla kutoka kwa mijadala hii katika mipango yake na kazi ya baadaye. Mwendeshaji ataongoza vikundi vyenu kupitia msururu wa maswali ili kuchunguza mawazo yenu juu ya ufaulu na fursa za wanafunzi, na jinsi wilaya, jumuiya, na Jimbo zinavyoweza kushirikiana pamoja ili kufanikisha aina ya fursa tunazotaka kuona shuleni.

Tafadhali kumbuka: Tunatambua kuwa elimu ni suala linaloweza kuibua hisia na maoni makubwa na haya ni mazungumzo yenye changamoto. Mazungumzo yetu jioni ya leo yatalenga kufafanua mafanikio kwa wanafunzi wetu na jinsi Shirika la Elimu linavyoweza kusaidia shule ili kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anapata fursa za elimu bora.

Tunaomba wale waliohudhuria kikao cha leo kuheshimu maoni tofauti tofauti kutoka kwa kila mmoja na kutambua kwamba kila mtu hapa jioni hii amekuja kwa sababu wanapania kuleta mabadiliko mazuri.

Maswali ya Majadiliano ya Kikundi

Mafanikio ya Mwanafunzi

1. Unapojua mwanafunzi amefanikiwa, inaonekanaje katika ngazi tofauti za elimu, ikiwemo:
    a. Shule ya msingi?

    b. Shule ya upili?

    c. Baada ya elimu ya shule ya upili?

2. Unapofikiria kuhusu mafanikio haya, ni data au taarifa gani unategemea kupima mafanikio ya:
    a. Mwanafunzi wako?

    b. Shule yako?

    c. Wanafunzi wa Vermont, kwa ujumla?

Usaidizi na Uzoefu wa Wanafunzi

3. Je, shule zenu zinasaidiaje wanafunzi kufaulu? (kwa mfano, elimu ya nje, mafunzo ya kijamii ya kihisia, usaidizi wa kimasomo, n.k.)

4. Je, kuna nyenzo nyingine ungependa kuona kwa wanafunzi ambazo hazipatikani kwa sasa?

5. Je, kuna kiwango cha chini cha fursa za elimu au uzoefu unafikiri unapaswa kupatikana kwa wanafunzi wote, bila kujali shule wanayohudhuria?

6. Je, unafikiri kuna vikwazo vya kutoa fursa hii ya chini katika mipangilio fulani?

Bajeti

7. Mifumo ya shule kote jimboni inakabiliwa na kupungua kwa usajili wa wanafunzi. Je, hii ni kweli katika mfumo wako na kama ni hivyo, umeona athari gani?

8. Baadhi ya shule katika jimbo zina idadi ndogo ya usajili ambayo inaweza kuzifanya ziwe ghali zaidi kuendesha na kuwa ngumu kuwapa wanafunzi anuwai kamili ya fursa za masomo. Hata hivyo, mipangilio hii mara nyingi ni muhimu kwa jamii na familia. Vermont inapaswa kusawazishaje mipangilio midogo na uhitaji wa fursa za elimu kwa wanafunzi?

9. Vermont ni jimbo linalothamini uhuru na udhibiti wa ndani linapokuja suala la elimu, lakini kunaweza kuwa na faida za kufanya kazi pamoja. Je, ni mambo gani ambayo ungependa kushiriki ili wanafunzi na shule ziwe na fursa zaidi kwa gharama ambayo ni endelevu?